JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI

**Dar es salaam**

15 Oktoba,2025

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), na Umoja wa Ulaya (EU) itazindua Viwango Fanisi vya Chini vya Nishati (Minimum Energy Performance Standards – MEPS) na Maabara za Upimaji wa Ufanisi wa Nishati utakaofanyika kesho tarehe 16 Oktoba 2025, katika Makao makuu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuanzia saa 4:00 asubuhi, na mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba .

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye makao makuu ya TBS jijini Dar es salaam Kamishna wa umeme na nishati jadidifu Mha. Innocent Luoga amesema kupitia ushirikiano kati ya Umoja wa Ulaya na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Serikali imeanzisha Maabara za kisasa za kupima matumizi bora ya nishati ndani ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), zenye thamani ya zaidi ya Euro milioni 1.8 (takriban shilingi bilioni 5).

Mha.Luoga amesema lengo ni kuhakikisha vifaa vya umeme vinavyotumika nchini vinatumia nishati kwa ufanisi kwa lengo la kupunguza gharama kwa watumiaji na kulinda mazingira dhidi ya uzalishaji wa hewa ukaa. Aidha, juhudi hizi zitasaidia umeme wa ziada kwenye gridi ya Taifa kutumika kwenye maeneo mengine ya nchi yenye upungufu wa umeme na kuweza kuwafikia wateja wengine wapya.

Maabara hizi zitakuwa na jukumu la Kupima na kuthibitisha ubora na ufanisi wa vifaa vya umeme vinavyoingizwa nchini, Kudhibiti bidhaa duni zisizo na viwango, Kutoa ithibati kwa wazalishaji wa ndani na Kusaidia Serikali katika usimamizi wa soko (*market surveillance*).

Viwango hivyo vitahusisha bidhaa za majokofu, majiko, mota za umeme, taa, vipoza hewa, na vifaa vingine vya umeme ili kupima ubora wa vifaa hivyo vitakavyotumiwa na

wananchi. Uzinduzi huu unaifanya Tanzania Kwa mara ya kwanza kuwa na uwezo wa ndani wa kuhakikisha bidhaa hizi zinakidhi viwango vya kitaifa na vya kikanda kabla ya kufika kwa mlaji.

Uundaji wa viwango hivi umehusisha Wataalam kutoka taasisi zaidi ya 10 zikiwemo Wizara ya Nishati, TBS, TANESCO, EWURA, REA, TIRDO, DIT, UDSM, ATC, NCC, TAREA na sekta binafsi.

Uanzishaji wa MEPS na maabara hizi unalenga kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Taifa (2015), Mkakati wa Taifa wa Matumizi Bora ya Nishati (NEES 2024–2034) na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Imetolewa na

Neema Chalila Mbuja
**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**